Teacher.co.ke

**Name ……………………………………………………………………………………………. Index No. ………………. Class …….**

# STAREHE GIRLS' CENTRE MOCK EXAMINATION 2025

**KISWAHILI FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**

**KARATASI YA 3: 102/3**
**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO**

a) **Jibu maswali manne pekee.**
b) **Swali la kwanza ni la lazima.**
c) **Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; tamthilia, riwaya, hadithi fupi na fasihi simulizi.**
d) **Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.**
e) **Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.**
f) **Majibu yote sharti yaandikwe kwa kijitabu cha majibu ulichopewa.**
g) **Andika nambari ya maswali uliyoyajibu.**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**USHAIRI**

a) Kupigania uhuru /haki /kujiendeleza kiuchumi
- Washiriki /walisimama /walitaka milki pamoja

(2 x1)

b) Kinaya
- Viongozi kujinufaisha -raia maskini.
- Viongozi kudharau raia -kuwatemea mate.
-Raia kupigania uhuru -kutofaidika.
-Kutoafikia maazimio -milki ya haki.
-Walianza safari pamoja -mwishowe wanabaguliwa.

(4 x 1=4)

c) i)Mizani -msuko -mshororo wa mwisho wa kila ubeti umefupishwa.
ii)Vina-ukara -vina vya kati vinabadilika vya tamati vinatirirka. (2x2=4)
(Kutaja 1 na kueleza 1)

d) Mshairi analalamika kuwa viongozi walipofikia hali nzuri ya Maisha tamaa ilizidi huku wakiwa na starehe za kila aina huku akiwasahau waliowapa nafasi za uongozi ili kufikia hali yao ya sasa.

(4x1=4)

e) Inkisari-Tukawa’chia -Tukawachia-kutosheleza mizani.
- Kuboronga sarufi -kialeni wadiriki -wadiriki kialeni -urari wa vina.
- Tabdila -shaki-shaka-urari wa vina
Lahaja /kikale -kialeni-kialeni-upekee wa msamiati /mapigo ya kimziki.

(za kwanza 2x2)

f) .
- Lina beti nane.
- Mishororo minne kwa kila ubeti.
- Mshororo wa mwisho umefupishwa katika kila ubeti.
- Msishororo wa kwanza hadi wa tatu katika kila ubeti vina vipande viwili.
- Kila mshororo una mizani kumi na sita na wa mwisho una mizani sita katika kila ubeti .
- Vina vya ndani havifanani ilihali vile vya nje vinafanana.( 4 x ½ = 2)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**
**Timothy Arege**
**BEMBEA YA MAISHA**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. (a.) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali.

Sara : Mimi ninashukuru kwa hawa alionipa mungu. Nikitaka zaidi nitakuwa mchache wa shukrani.(kimya) Dina nimesemwa sanana kutukanwa kwa sababu ya hawa wasichana wangu. Wewe unajua yote yaliyosemwa, hadharani na faraghani. Si makanisani, si magengeni. Leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao, ninaridhika moyoni. Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika. (Anatokwa na machozi)

Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha.

i.) Changanua maudhui katika dondoo hili (ala 3

- suala la jinsia / ubaguzi wa kijinsia – Sara antukanwa kwa kupata watoto wa kike.
- Dhuluma – Sara kutukanwa kwa sababu ya kupata watoto wa kike.
- Uwajibikaji – Watoto wa Sara wanajiendeshea mambo yao.
- Imani katika dini/ Dini – Sara anamshukuru Mungu kwa watoto aliompa.
- Mabadiliko
- Malezi
- Kutokata tamaa
- Maadili
- Bidii

3 x 1 = 3

ii.) Bainisha toni katika dondoo hili

- Toni ya huzuni/ masikitiko : Sara anatokwa na machozi.
- Toni ya kulalamika – Sara analalamikia kutukanwa.
- Toni ya ukakamavu – Sara anafurahia hali ya watoto wake kujitegemea.
- Toni ya kuridhika – Ameridhika. Yu tayari hata kufa.
- Toni ya utulivu. (ala 2)

iii.) Tambua mbinu tatu za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (ala 3)

- kuzungumza moja kwa moja na mnenewa – Dina nimesemwa…
- tanakuzi – faraghani – hadharani/ leo – jana.
- Tabaini – si makanisani si magengeni.
- Tasfida – hata nikiitwa / badala ya hata nikifa
- Usambamba – si makanisani, si magengeni.
- Matumizi ya nafsi ya kwanza – mimi ninashukuru kwa hawa alionipa Mungu.
- Kejeli – vitoto.
- Ulinganishi – walipokuwa watoto na sasa wamekuwa watu.
- Taswira – anatokwa na machozi.
- Stihizai / dhihaka – kudharauliwa na sasa ni watu.

(b.) Jadili jinsi suala la utu linavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea Ya Maisha(ala 12).

- Wazazi kuwajali wana wao. Sara anamweleza Yona kuwa hafai kutarajia mengi kutoka kwa Neema kwani anashughulikia mahitaji mengi./ Dina kumjali.
- kusaidiana katika kazi – Dina anaenda nyumbani kwa Sara kujulia hali na pia kumpikia chakula.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

- Watoto kuwashughulikia wazazi – Bunju na Neema wanawajengea wazazi wa Neema Nyumba kijijini.
- Ndugu kuwajali wenzao – Neema anawasomesha wanuna wake.
- Kujitolea katika kutekeleza majukumu – Bunju anajitolea kugharamia mahitaji yote ya nyumbani ili Neemea ashughulikie mahitaji ya wazazi na wanuna wake./ Neema kununulia wazazi gesi.
- Ukarimu wa majirani – Luka anawakaribisha wazee wanzake ili washiriki chakula , vinywaji na mazumnumzo.
- Wazazi kuwalea wana wao kwa njia inayofaa. – Yona na Sara, Bunju na Neema wanatekeleza majukumu yao ya malezi ya wana kwa kuzingatia maadili.
- Utu wa Bunju – Bunju kumsaidia Neema alipohusika kwenye ajali.
- Upendo na ukarimu miongoni mwa wanandoa- Bunju anamnunulia Neema gari hata ingawa Neema ana kazi yenye ujira./ Sara anamsaidia Yona katika malezi ya wana wao anapofutwa kazi.
- Bunju anamtuliza Neema anapohisi kuwa amemuumiza kihisia kwa kumkumbusha wema aliomtendea.
- Neema anawaajiria wazazi wake wafanyakazi.
- Neema anamwendea mamake kwa gari.
- Sara anavumilia ulevi wa Yona
- Bella kusaidia katika shughuli za ujifunzaji, anamsikiliza Lemi akiimba.
- Neema anapomtoa mamake kijijini anampeleka moja kwa moja hadi nyumbani mwake kupumzika.
- Kuwachukulia wenzao majukumu – Dina kumkatia Sara tikiti mara kwa mara.
- Sara kutomuumbua mumewe mbele ya wanawe.
- Sara kuwashauri Asna na Neema kutomhukumu Bunju.
- Sara kumwonya Asana dhidi ya kuingilia uhusiano wa Neema na Bunju.
- Yona kuomba msamaha kwa familia yake.
- Luka namwonya Beni dhidi ya kufurahia machungu ya wengine huku yeye akihisi vibaya anapotajiwa yake.
- Kudumisha mahusiano  mema – akina Beni wanashirikiana kunywa pombe.
- Bunju kumsomesha salome.
- Neema kushughulikia matibabu ya wazazi.
- Sara kumjali mumewe – amamtetea kwamba amejaribu.
- Asna kumkaribisha mamake kwake na kumpikia uji.
- Bunju kukubali kuishi na Salome akisoma.

Hoja 6 x 2 = 12

**3**. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. (ala 20)

Zozote (20 x1) ( alama 20)

**Majibu**

1) Kutoka  ujana hadi uzee – Yona
2) Sheria kubadilika – katika Elimu. Huwezi kumnyoosha mtoto kwa  Kiboko.
3) kubadilika kwa mtazamo. Yona anabadilisha mtazamo wake kwa sara na kumwelewa kuwa alikuwa mgonjwa.
4) Kubadilika kwa hisia.- Yona analalamikia Sara kwa kutopika lakini baadaye anamhurumia.
5) Yona anabadilisha hali yake ya zamani na kuamua kufuata mkondo mpya wa maisha.
6) Yona anasawiriwa kama mtu mzuri mwanzoni, lakini baada ya kusutwa na kudharauliwa.
7) Yona anabadilika na kujutia ulevi wake kuwa pombe ilimchezesha kama mwanasesere.
8) Kuna mabadiliko kuhusiana na mila na desturi – kuhusiana na mtoto wa kike na wakiume.
9) Katika kizazi cha leo mtoto wa kike anaweza kurithi na kushughulikia wazazi wao.
10) Ndoa inakumbwa na mabadiliko – mtu hujichagulia wakati wa kuoa/ kuoelewa kinyume na hapo awali msichana alipolazimishwa.
11) Majukumu vilevile yanabadilika Yona anaingia jikoni kumpikia Sara.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

12) Mbeleni wazee walifunzwa na dunia lakini kizazi cha leo kinategemea vitabu tu ili kufahamu lolote.
13) Hali ya uchumi inabadilika – wanaotegemea mifuko yao watakabiliana na kipindi kigumu.
14) Mitindo ya nyimbo-
15) Burudani – watoto wa kisasa hupenda kupelekwa out.
16) Elimu ya sasa haina mafundisho kwa vijana kuhusu ndoa.
17) Mbeleni watoto walifunzwa na kuzishikilia mila na desturi ila sasa wamwezitupa mila na desturi zao.
18) Watoto walitumia lugha asilia, leo hawajui hata neno moja.
19) Zamani wasichana hawakuendelea na masomo.
20) Safari za kwenda kijijini hazibughudhi kama zamani kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia.

(zozote 20 x 1)

**SEHEMU YA C: RIWAYA**

C. MOMANYI: **NGUU ZA JADI**

**Jibu swali la 4 au la 5**

Majibu :

**4. ) "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."**

**(a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)**

i) Huu ni uzungumzi nafsi wa Mangwasha

ii) Mangwasha anarejelea mabadiliko ya Mrima ya kunywa pombe

iii) Hii ni baada ya Mangwasha kukata kauli kuchunguza sababu za Mrima kuanza kunywa pombe.

iv) Mangwasha yupo nyumbani.

**(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano.(alama 5)**

i) Mangwasha anaonyesha ujasiri pale anapojitahidi kwa jino na ukucha kuiokoa ndoa yake kutoka kwa Sagilu aliyekuwaakiisambaratisha. Kule kumsaka mumewe kwenye mabanda ya uuzaji wa pombe mbali na kukabiliana na walevi ni ishara ya ujasiri (uk. 34-36).

ii) Ujasiri wa kuiokoa ndoa yake unaonekana pia pale anapoandamana na Lonare, Sauni na wengine kumsaka mumewe Majaani, pahali palipojulikana kuwa hatari kwa sababu paliishi watu waliotindikiwa kimaadili.

iii) Mangwasha anaonyesha ujasiri pale anapochukua barua ya Chifu Mshabaha na kwenda kuirudufu kinyume na idhini yake ilimradi apate ushahidi wa kuweza kushinda kesi yao ya ardhi. iv) Tofauti na waajiriwa wengine wanapofutwa kazi, Mangwasha anamkabili Chifu Mshabaha kwa ujasiri na kumwita mkabila mkubwa (uk. 136).

v) Ujasiri wa Mangwasha pia unaonekana aliposimama mbele ya kaumu na kuwahamasisha Waketwa wenzake kurudi katika ardhi yao ya Matango. Hakujali mila wala vitisho vya waliowapokonya ardhi yao bali aliwahamasisha warudi katika ardhi yao ambayo ilikuwa haki yao.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

vi) Lonare anapopatikana nje ya nyumba yao baada ya kutekwa nyara, tunamwona Mangwasha akimkimbilia licha ya kwamba kulikuwa na umati mkubwa na hakuna aliyejaribu kumsogelea kutokana na hofu iliyowapata (uk. 170). Anaungana na

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

wanaume kama Lonare, Sagura na Sauni ili kuikomboa nchi yao kutoka kwa utawaladhalimu, bila kujali mikatale ya utamaduni wake.

**(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaana ubinafsi katika nchi ya Matuo. (alama 11)**

i) Mtemi Lesulia anajawa na tamaa ya uongozi. Yuko tayari kuwadhulumu au hata kuwaua wapinzani wake kutokana na tamaa ya uongozi wa nchi. Anamteka nyara Lonare asiweze kuwa katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu anapohisi kwamba huenda akamshinda na kuwa mtemi (uk.10, 51, 164-172).

ii) Aidha, akiwa na wakwasi wenzake kama vile Sagilu na Mbwashu wanahujumu pato la nchi kutokana na tamaa ya kujilimbikizia mali. Ubinafsi wa Mtemi Lesulia unaonekana pale anapomiliki rasilimali za serikali hasa kupitia kwa unyakuzi unaoendelezwa na mkewe Nanzia.

iii) Mfano unaotolewa wa mchwa na kichuguu (uk. 93) unaonyesha pia ubinafsi wa mtemi kutokana na kufaidi jasho la wengine. Nanzia anaonyesha tamaa na ubinafsi pale anapojaribu kubinafsisha jumba la Skyline Mall ambalo ni mali ya serikali (uk. 147)na ardhi ya Matango kwa kushirikiana na mafisadi wenzake.

iv) Sagilu anaendeleza maudhui ya tamaa na ubinafsi pale utashi wake wa pesa unampofanya kuhodhi bidhaa kama vile ngano ili kuiuza kwa bei yajuu (uk. 17). Tamaa hiyo inamfanya hata kuhatarisha maisha ya watoto nchini Matuo anapoagiza maziwa yenye sumu kutoka ughaibuni (uk. 17). Ubinafsi wake unamfanya kuwazuia wengine wasimpiku kibiashara.

v) Tunaambiwa, "Kwa wale waliomshinda kwq werevu, aliwafanyia hila, mizungu na visanga hata kuwafilisi kabisa kibiashara." (uk. 16). Tamaa ya uongozi na mali inamwingiza katika urafiki na mtemi ili kutosheleza maslahi ya kibinafsi. Ubinafsi pia unamfanya Sagilu kumtumia Mrima ili kujinufaisha kisiasa kutokana na tamaa ya uongozi. Sagilu aliandamwa pia na tamaa za kimwili. Anawabadilisha wanawake hadi kuitwa dudumizi kutokana na kuvizia na kuwachukua wake wa wengine (uk. 18

vi) Kupitia kwa Sagilu pia, tunamwona akiendeleza ubinafsi kwa jinsi anavyomtumia Sihaba Sio tu kama kimada wake bali pia kutosheleza utashi wake wa kumiliki mali na biashara.

vii) Anaendeleza maudhui ya tamaa anapomnyemelea Mangwasha tangu pale alipokuwa msichana hadi baada ya kuolewa na Mrima ili kutosheleza uchu wake. Tamaa ya Sagilu inamfanya hata kuzaa na mke wa Mtemi Lesulia kutokana na udhaifu uliodhihiri katika ndoa yake. Anatumiwa pia na mtemi kama kikaragosi ili kuwanyanyasa watu wa Matango huku akitumaini kufaidika kibinafsi.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

viii) Mrima anaendeleza maudhui ya tamaa na ubinafsi pale ambapo tamaa ya pesa inamtosa katika tabia potovu. Anadanganywa na Sagilu huku akipewa pesa hadi kuitelekeza jamaa yake. Ubinafsi wa kuyajali maslahi yake pekee unamfanya kukaidi masharti ya ndoa na uwajibikaji.

ix) Ubinafsi wa Mafamba unamfanya kuhujumu sheria za nchi kwa kuutetea ufisadi serikalini. Ubinafsi pia unamfanya kudanganya kuwa vyeti vya kumiliki ardhi vya wenyeji wa Matango vilikuwa ghushi (uk. 94), na kwamba serikali ilitaka kujenga soko katika mtaa wa Matango.

x) Tamaa ya pesa inamfanya Sihaba kujiingiza katika biashara ya ulanguzi wa watoto wa kike (uk. 141-144). Usuhuba wake na Sagilu pia unajengwa juu ya misingi ya tamaa ya pesa na ubinafsi. Anatumiwa na Sagilu kuhujumu haki za Waketwa mbali na kutumiwa na Sagilu kuwaangamiza maadui zake kibiashara (uk. 16). Hakujali maslahi ya wengine ila yake binafsi.

**5.) "Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa nguvu akajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe. Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunzawaja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia piahujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.**

**(a) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 5)** i) Uzungumzi nafsi - Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu

ii) Taswira sikivu – alishusha pumzi kwa nguvu. iii)Swali balagha – kuna Osama kuliko huyu

1. Jazanda – kuna Osama kuliko huyu
2. Kinya - Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunza waja.
3. Takriri – neno maovu limerudiwa
4. Tanakuzi – waliomo na wasiokuwemo .
5. Mdokezo wa methali - Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**(b) Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuzaRiwaya ya Nguu za Jadi**

**(alama 5)**

i) Mandhari haya yanaibua maudhui ya ndoa – Mangwasha ameolewa na Mrima na wana watoto wawili.

ii) Mandhari haya yanachimuza maudhui ya utabaka - bwanyenye mmoja anayetaka ardhi mjini Taria anasababisha moto unaofurusha akina Mangwasha.

iii) Mandhari haya yanamjenga mrima kama hatari kwa usalama – Mangwasha anajisemea kuwa hakuna mtu hatari dunia kama Mrima . anamlinganisha na Osama.

iv) Mandhari haya yanaonyesha uhasama wa jamii za nchi ya Matuo. Zamani Waketwa na Wakule walizozania mifugo wakawindana na kupokonyana mifugo.

v) Mandhari haya yanaibua maudhui ya chuki – chuki iliwavaa wakule, hata ukame na njaa viliposhamiri, waketwa waliandamwa na kumiminiwa lawama.

vi) Mandhari haya yanachimuza maudhui ya ufisadi – tunaambiwa kuwa chifu mshabaha alikuwa amepokea mlungula huku ardhi ikinyakuliwa.

vii) Maandhari haya yanaibua nafasi ya mwanamke katika jamii – mwanamke alitakiwa kusikiliza na kutenda bali si kusikilizwa na kutenda.

**(c) Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawakatika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi.**

**(alama 10)**

i) Dhana ya kwamba mwanamke ni chombo tu cha kuchuuzwa na mwanamume inajitokeza katika uk.10 pale ambapo baadhi ya Waketwa waliochomewa nyumba zao wanatoa hoja kuwa kuna wale waliowauza wake zao kwa wakuu ili wapate ajira.

ii) Wanawake hawana sauti mbele ya wanaume kama anavyowaza Mangwasha kuwa "...walipaswa kusikiliza na kutenda bali si kusikilizwa na kutenda." (uk. 11). Maudhui haya yanaendelezwa pia na mhusika Mangwasha tunapojulishwa kuwa utamaduni uliomlea ulimfunza kutotumia sifa za kike kustarehesha wanaume ili kujinufaisha kimaisha.

iii) Utamaduni unamfunza mke kujitegemea katika maisha bali si kumtegemea mume kujikimu katika maisha yake (uk. 12). Udanganyifu ili kufaidi kitu pia hauvumiliki kwa mwanamke na mila inayozingatiwa na jamii inabainishwa vyema na mhusika Mbungulu anaposema, "Usimfuate mumeo kwenye makao ya starehe." (uk. 32).

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

iv) Maudhui ya imani asili ya jamii pia yanakaririwa na Mrima anayeamini kuwa mwanamke huwa na maneno mengi kama chiriku (uk. 40) na kwamba mke hapaswi kumuuliza mumewe kule aendako au atokako. Mrima anasema, "...wanawake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee." (uk. 40). Mifano anayotoa Mrima ya 'ngamia kumea pembe' au 'shingo kupita kichwa' ni ishara kamili ya jinsi utamaduni asilia unavyomfunza mwanamume kuhusu mwanamke kumaanisha daima mwanamke hawezi kumpiku mwanamume.

v) Kupitia kwa Mrima pia, maudhui ya jinsi utamaduni asilia unavyosawiriwa katika riwaya yanaonekana pale anaposema kuwa yeye ni mwanamume na mke hangemzuia kuoa; kwamba angeweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake. Katika jamii nyingi hasa barani Afrika, wanaume huweza kuoa zaidi ya mara moja na hii ni desturi kongwe miongoni mwa jamii nyingi.

vi) Utamaduni asilia pia unamtaka mume aweze kuitunza jamaa yake pamoja na kuisimamia. Hii ndiyo maana Mrima anasisitiza kuwa mila haimruhusu kutunzwa na mkewe. Anasema, "Siwezi kuvunja mila kwenda kutunzwa kama mtoto." (uk. 101). Haya yanakaririwa na Sagilu anapomuuliza Mangwasha kwa nini hajamwambia ampe Mrima kazi. Hii inamaanisha si ada ya mume kutunzwa na mke. Dhana ya uovu wa mwanamke ni dhana inayoshikiliwa na jamii nyingi pia ulimwenguni. Dhana hii inaendelezwa kupitia kwa kisasili anachosimulia mhusika Sauni kinachobainisha uovu na kutoaminika kwa mwanamke (uk. 80-83).

vii) Utamaduni wa kisasa unajitokeza kwa sura mbalimbali. Desturi ya kuhodhi mali na kujilimbikizia pesa inatokana na ubinafsi unaofungamana na maisha ya kibepari. Mashindano ya kujinufaisha kifedha na uchu wa kuwa na mali nyingi au vitu ndio unaowafanya watu kutoweza kuwajali wengine hasa matajiri. Jamii inajigawa katika makundi mawili; walio navyo na wasio navyo.

viii) Desturi ya mali kumilikiwa na wachache kama vile akina Sagilu, Mbwashu na jamaa ya Mtemi Lesulia inaendeleza ubeberu na unyanyasaji wa maadui wao. Usasa pia unabainika kutokana na wingi wa maisha ya raha na starehe. Jamii inazingatia maisha ya ufasiki, uzinzi na kutowajibika katika ndoa. Tunaambiwa Sagilu anabadilisha magari sawa na anavyobadilisha wanawake (uk. 18). Ngoswe pia anakumbatia maisha ya anasa na biashara haramu kama ile ya mihadarati

ix) Wasichana wanatupilia mbali maadili na kukumbatia starehe na pesa kuliko utu kama vile Sihaba na Cheiya. Majukumu katika asasi ya ndoa yanabadilika. Pale ambapo mwanamume anahitaji kuwa kichwa kwa jamaa yake, tunamwona akihepa jukumu hili linalotwaliwa na mwanamke hasa katika ndoa za kisasa. Hivi ndivyo anavyofanya Mangwasha (uk. 29).

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

x) Wanaume nao wanakosa adabu wanapowanyemelea wake za watu. Tazama jinsi Sagilu anavyomnyemelea Mangwasha au hata kuzaa na mke wa Mtemi Lesulia (uk. 161).

xi) Mangwasha anaonekana kukashifu mila zilizopitwa na wakati pale anapomwambia Mbungulu kwamba angeivunja mila ya kutomfuata mumewe katika starehe zake (uk. 32) na kudharau baadhi ya mila kama hizo.

**SEHEMU YA D :HADITHI FUPI**

*MAPAMBAZUKO YA MACHWEONA HADITHI NYINGINE*

*Jibu swali la 6 au 7*

## Hadithi fupi.Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingineo.Sabina.

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika

***Mrejelewa ni Sabina***

i) Ametumiwa kuendeleza na kukuza ploti ya hadithi kutokana na mgogoro baina yake na familia ya Ombati..
ii) Ni kielelezo bora cha wanajamii wanaoenzi masomo na wanaojitolea sabili ili kupata ufanisi katika maisha yao ya halali.
iii) Mwandishi amemtumia kukashifu ukiukaji wa haki za watoto na kukandamizwa kwao.
iv) Ametumiwa kudhihirisha maudhui ya uwajibikaji, elimu na ukiukaji wa haki za watoto mayatima.
v) Ametumiwa kudhihirisha matatizo yanayopitiwa na watoto mayatima.
vi)Amechimuza sifa ya Ombati na Yunuke kama katili.
v) Ametumiwa kufanikisha methali baada ya dhiki faraja kwani anajipitia magumu mwanzoni lakini baadaye maisha yake yanaendelea.(uk. 94), na kwamba serikali ilitaka kujenga soko katika mtaa wa Matango.
vi) Anatambulisha wahusika kwa mfano Yanuke,Ombati n.k (alama6x1=6)

b) Aina za taswira katika kifungu.
i) Taswira sikivu mfano,...yalimwiingia Ombati maskioni.
ii) Taswira oni mfano,…amevaa rinda kuukuu,walimzoa juujuu,kupigwa picha.
iii)Taswira mnuso mfano,…harufu ya samadi inamvuka.
iv)Taswira mguso mfano,…walimzoa juujuu. (alama 4x1=4)

## (c)Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi

- Wanajamii kumtenga Sabina wakidai familia yao iliandamwa na mikosi na nuksi.
- Sabina kudhulumiwa kwa kupigwa na Yunuke.
- Sabina kusongwa na mawazo kabla ya mtihani wa kitaifa.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

- Sabina kupangiwa njama ya kuozwa mapema hata kabla ya kumaliza masomo yakc(wa darasa la nane )kuwadia.
- Sabina kufanyishwa kazi za sulubu na Yunuke.
- Nyaboke (mamake Sabina ) kupata ujazito akiwa umri mdogo.
- Sabina kulelewa na mzazi mmoja akiwa na umri mdogo.
- Nyaboke kulazimika kuacha shule baada ya kupata mimba.
- Babake Sabina kumkana Sabina baada ya kumkana Sabina mchana peupe.
- Sabina kuachwa yatima baada ya kifo cha mamake. Analazimika kuishi na babu na nyanya.

Sabina kudhulumiwa na Yunuke na kuambiwa kuwa juhudi zake katika masomo hazitafanikiwa. (alama 10x1=10)

6. **SWALI LA MZIMU WA KIPWERERE**

a)Maneno ya msimulizi Akimrejelea Bishoo

Yuko mzimuni wa Kipwerere
Msimulizi alikuwa amewafumania Bishoo na Salihina katika mzimu ambako alipata makasha ya tubako,robota ya bangi na mitungi ya chang'aa.

(alama 4x1=4)

b i) Kubainisha mgogoro katika hadithi – mgogoro uliopo unaotokana na itikadi unaotumiwa na kina Salihina kuwalaghai wanakijiji.

ii) Kuwatambulisha wahusika. Bishoo na Salihina

iii) Kuchimuza maudhui:ulaghai – Salihina anajifanya kuwa mdumishaji wa maadili ilhali yeye ndiye alikuwa akilangua dawa za kulevya.

iv) Kutambulisha sifa za wahusika: Bishoo anabainika kuwa mwongo kwa kuwa anamdanganya mumewe kuwa alikuwa akienda kumwona mtoto mgonjwa ilhali alikuwa anaenda kwa Salihina.

v) Kuibua dhamira ya mwandishi: Kuonyesha madhara ya ushirikina na itikadi: imani kuhusu Mzimu wa Kipwerere unawatia wanajamii hofu ilhali hakukuwa na mizimu au mashetani yoyote katika kichaka hicho.

vi.Kuendeleza ploti – kusuluhisha taharuki kuhusu kuwepo kwa mashetani katika mzimu kwa kuonyesha kuwa hakukuwa na shetani yeyote ila wajanja kama kina Salihina.

**Zozote 4 x 1 = 4**

c i) Tashbihi …meupe kama ya maiti, mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama."

ii)Taswira oni… maguo yangu meupe (alama 2x1=2)

d i)Inaaminika kuwa yeyote aliyekiuka miiko kuhusu kutoingia katika mzimu angetolewa kama kafara kwa mizimu.

a) Wanajamii wa eneo la Mzimu wa Kipwerere wanaamini kuwa Salihina angeweza kuwasiliana na mizimu. Hivyo, wanapotaka kuandaa sherehe kama vile jando wanamtuma Salihina kuzungumza na mizimu.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

b) Kuamini kwamba mwanamke na mwanamume waliozungumza walikuwa shetani na mkewe. Inadaiwa kuwa waliungumza wakati watoto wao walikuwa wamelala.
iv)Mashetani wanavuta sigara - Kuamini kwamba harufu ya sigara iliyotoka katika mzimu ilitokana na shetani aliyekuwa akivuta sigara.
v) Kuamini kwamba kulikuwa na wimbo uliokuwa kama ufunguo wa kuingia katika mzimu.
vi) Kuna itikadi kuhusu chanzo cha kichaka cha Mzimu wa Kipwerere – inaaminika kuwa kichaka hicho kilitokana na kaburi la mwanamke aliyeitwa Kipwerere.
vii)Wanajamii wa eneo la Kipwerere kutoruhusiwa kupita kichaka hicho saa sita mchana na usiku wote. Wanajamii hawakupewa sababu zenye mashiko za kuwanyima ruhusa ya kupitia kichaka hicho bali walitishiwa tu kuwa wangetolewa kama kafara kwa mzimu.
vii) Kuamini kwamba taa zilizowaka usiku katika Mzimu wa Kipwerere ziliwashwa nashetani wa mzimu ili kuwapa watoto wake chakula.

## SEHEMU YA E: FASI HI SIMULIZI

*Swali la nane*

**FASIHI SIMULIZI**

Swali la nane

a) i) Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee. Ni utumiaji walugha kwa mvuto na ufasaha. ( alama 2x1=2)

ii) i)Hukuza uwezo wa kujieleza hadharani
ii)Hukuza ujuzi na ufasaha wa lugha
iii)Msingi wa kuteua viongozi
iv)Huhifadhi utamaduni wa jamii
v)Huburudisha
vi) Hukuza uzalendo
vii) Huweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu
viii)Ni kitabulisho cha utabaka

iiii) a)Dhamira – lengo/nia inayokusudiana na hadithi b)i.)Maudhui- mambo yanayoelezwa katika hadithi k.m hekaya
ii.)Ploti – mtiririko wa utushi ama tukio katika hadithi.
iii.) Mandhari- mazingira ya wakati , hali au kimaeneo. Ya kuogofya, yenye misitu namajitu au mazimwi.
iv.)Wahusika- viumbe wa hadithi wa aina gani.

v.)Usimulizi- hadithi inasimuliwa katika nafsi ya kwanza au ya tatu.
g)Muundo- miundo maalum ya kuanza na kufunga hadithi
vi.)Lugha- lugha ya moja kwa moja (sahili) na inayoweza kutumia tamathali za lugha.
(za kwanza sita 6 x 1= 6)

b) i) kuuliza maswali
ii) kujibu maswali
iii) kuwahusisha katika nyimbo
iv)kucheka pamoja
v)Kupiga makofi
vi)Kushangilia vii)mdokezo

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

viii) Kuuliza maswali ya balagha ili kuibua hisia

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ix.) Mtuo wa kidrama.

x.)kuvaa maleba

x.) Ala za muziki.

Zozote 6 x 1 = 6

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes